

SHULE YA UPILI YA GATITU, S.L.P. 327-01030, GATUNDU.

HAMASISHO : KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI (2015)

JINA.....DARASA.....NAMB:.....

A) Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata

Kijana wetu maridadi kesho na ije,
Nitakutia nambari,
Ndio, nitakutia nambari.

Kijana maridadi nakwambia usilie,
Na ije kesho utatiwa nambari,
Ndiyo utatiwa nambari.

Ni leo na kesho kijana maridadi,
Na ije kesho utatiwa nambari,
Ndiyo utatiwa nambari.

Nakwambia kisikupate kihoro kijana maridadi,
Na ije kesho utatiwa nambari,
Ndio,ni kweli utatiwa nambari.

MASWALI:

a) Huu ni wimbo wa aina gani? (Alama 1)

b) Wimbo wa aina hii huimbwa wakati gani? (Alama 2)

c) Taja na ufafanue mbinu **MOJA** ya lugha iliyotumika katika utungo huu. (Alama 1)

d) Eleza dhima **TATU** za wimbo wa aina hii katika jamii. (Alama 3)

e) Onyesha udhaifu wa nyimbo katika jamii.

(Alama 2)

.....
.....

B. 1) Eleza sifa **NNE** bainifu za kimuundo za methali.

(Alama 4)

.....
.....
.....
.....

b. Mianza ya hadithi huwa na umuhimu gani katika masimulizi?

(Alama 2)

.....
.....
.....

B. HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI ZINGINE

Swala la mapenzi na ndoa ni swala nyeti katika jamii. Fafanua ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi zifuatazo : *Shaka ya mambo, Kanda la usufi na Ndoa ya zamani*

(Alama 15)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....